# #AkiliYaDiamond

MAMBO 50 USIVYOJUA KUHUSU
AKILI YA DIAMOND

KIPAJI, UBUNIFU NA MAFANIKIO

*Godius*

*Rweyongeza*

*(SONGAMBELE)*

**Vitabu Vingine Vya Mwandishi Huyu**

1. Kutoka Sifuri Mpaka Kileleni
2. Tatizo Si Rasilimali Zilizopotea (Toleo La Kwanza Na La Pili)
3. Nyuma Ya Ushindi.
4. Mambo 55 Ya Kuzingatia Kabla Ya Kuanzisha Biashara.
5. Jinsi Ya Kuibua Ubunifu Ulio Ndani Yako.
6. Kama Unataka Kuwa Tajiri.
7. Barua Ya Wazi Kwa Wazazi Na Walezi Wa Watoto.

8. Makosa Kumi (10) Wanayofanya Wakulima Na Jinsi Ya Kuyaepuka Ili Kutengeneza Fedha Zaidi.
9. Maajabu Ya Kusoma Vitabu (toleo lililoboreshwa zaidi)
10. Maajabu Ya Kuweka Akiba
11. Tofauti 50 Kati Ya Matajiri Na Masikini

# AKILI YA DIAMOND

Mambo 50 Usiyoyajua Kuhusu Akili Ya Diamond

KIPAJI, UBUNIFU NA MAFANIKIO

Godius Rweyongeza

Akili Ya Diamond

©GODIUS RWEYOGEZA

Agosti 2020
MOROGORO, TANZANIA

Haki zote zimehifadhiwa
Hakuna sehemu yoyote ile ya kitabu inaruhusiwa kutolewa upya, kunakiliwa au kuhamishwa kwa namna yoyote ile. Iwe ni kwa njia zinazofahamika sasa hivi au zitakazogunduliwa hapo baadaye bila idhini ya mwandishi.

*Akili ni kile unachobaki nacho baada ya kusahau yote uliyojifunza ukiwa shuleni*-Albert Einstein

# UTANGULIZI

Katika pitapita zangu hapa mtaani, juzi niliwasikia watu wanasema kwamba kama wangekuwa na akili kama ile ya Diamond aliyonayo kwenye kuimba, basi wangeweza kufanya mambo makubwa. Moyoni mwangu nikawa nasema, yaani, laiti mungejua kuwa mna uwezo kama huo na zaidi pengine msingesema hivyo, badala yake mngeenda kuutumia huo uwezo. Hivyo, leo hii nimeona nikushirikishe kiufupi kuhusu hii Akili Ya

Diamond. Sasa labda kabla hujaanza kusoma kurasa za ndani kabisa, nikuulize swali. Je, ungependa kuwa na Akili Ya Diamond au hutaki kabisa?

Naomba uandike jibu lako pembeni. Mwisho mwa kitabu hiki nimerudia kuuliza swali hilihili. Nitapenda ulinganishe majibu yako yote mawili. Hili ambalo unatoa hapa na hilo ambalo utatoa mwishoni mwa kitabu hiki.

*Godius Rweyongeza*

Morogoro-Tanzania

# 1. AKILI YA DIAMOND INASEMA KWAMBA UNAPASWA KUCHAGUA ENEO MOJA AMBALO UTAFAHAMIKA NALO

Kuna watu wapo vizuri sana kwenye kujaribu vitu vingi kweli. Unakuta kwamba wanajaribu biashara hii wanaachana nayo baada ya muda mfupi, kwenda kuanzisha biashara nyingine.

Kwao kila kitu ambacho kinaitwa fursa

WANAKIJARIBU. ila Akili Ya Diamond inatuambia kwamba unapaswa kuchagua kitu kimoja ambacho utafanyia kazi kisha vitu vingine unaviweka pembeni. LAKINI pia akili hii hapa inatukataza kujaribu, badala yake inakutaka ufanye au usifanye ila sio ujaribu.

Najua na wewe ukiulizwa kutaja kitu kimoja kuhusu Diamond utaenda moja kwa moja kutaja kuhusu muziki wake, basi.

Lakini je, watu wakiulizwa kutaja kitu kimoja kuhusu wewe watataja nini? na je, wewe mwenyewe ukiulizwa utaje kitu kimoja kuhusu wewe utataja kitu gani? INAWEZEKANA wewe mwenyewe hujijui. kwa hiyo basi chagua eneo moja ambalo utashughulika nalo, kiasi kwamba watu wakiwa wanataja jina lako basi kitu ambacho kitakuwa kinakuja kwenye akili zao iwe ni hicho ulichochagua. Je, kitu chako kimoja ni kipi? Ni uchoraji? Uimbaji? Uigizaji?

Uchekeshaji? Biashara? Mpira? Kwa vyovyote vile, chagua kitu kimoja, kisha kifanyie kazi kitu hicho hapo. na hiyo ndio Akili Ya Diamond

# 2. AKILI YA DIAMOND INAKUHITAJI UIFAHAMU SHERIA YA 80/20

Kanuni ya 20/80 inasema kwamba asilimia 20 ya vitu unavyofanya ndivyo vinakuletea matokeo makubwa ambayo ni sawa na asilimia 80,wakati asilimia 80 ya vitu unavyofanya inakuletea matokeo madogo ambayo ni sawa na asilimia 20 tu. Sasa Akili Ya Diamond inakuhitaji wewe ushughulike na vitu

vichache ambavyo ni sawa na asilimia 20 ila vinakupa matokeo makubwa ambayo ni sawa na asilimia 80. Hii ndio Akili Ya Diamond. Na wewe unapaswa kuitumia kwa manufaa yako

# 3. AKILI YA DIAMOND INAKUHITAJI KUONGEZA UBUNIFU KWENYE KAZI YAKO

Kwa kitu chochote kile ambacho utaamua kufanya, unapaswa kufahamu kuwa kuna watu wengine ambao watakuja kufanya hicho kitu hata kama wewe ndio kwanza kuanzisha hicho kitu. Au kama wewe sio wa kwanza kwenye hicho kitu basi maana yake watakuwepo watu wambao tayari wanafanya hicho kitu.

Sasa Akili Ya Diamond inakuhitaji wewe kuongeza ubunifu na kujenga jina lako.

Yaani, watu wakisikia kazi yako wajue kweli kwamba kutokana na upekee wa hii kazi basi, lazima mkono wa fulani hapa unahusika.

Na hii ndio akili anayotumia kwenye mziki, anajua kuwa wapo wanamziki wengi bila kuwa mbunifu, basi kazi yako haitapendwa na watu.

## 4. AKILI YA DIAMOND INAKUHITAJI WEWE KUFANYA KITU KWA UBORA WA HALI YA JUU SANA, HATA KAMA SIO CHA KWAKO.

Nimewahi kusikia mara nyingi kwa watu wengi wakisema kwamba ukimshirikisha Diamond kwenye wimbo wako basi ujue kwamba anaenda kukufunika. Hii ndio Akili Ya Diamond na wewe unapaswa kuwa na akili kama hii hapa. Yaani, pale utakapoenda

kushiriki kwenye kazi ya mtu basi hakikisha kwamba unaifanya kwa viwango vya juu kiasi kwamba kila mtu afurahie ushiriki kwako kwenye hiyo kazi.

Sio baada ya wewe kushiriki kwenye hiyo kazi ndio inakuwa kilio na karaha.

Yaani, watu wanaanza kujuta kwa nini walikushirikisha kwenye hiyo kazi. sio unaajriwa kwenye biashara watu wanaanza kujuta kwa nini walikuajiri kutokana wizi wako, uzembe, mihemko n.k.

Na hiki kitu ndicho kimekuwa kinafanya vijana wengi wanakosa ajira. Maana, wao wakipewa ajira wanawaza ni kwa namna gani wao watanufaika kwanza. Wanawaza ni kwa namna gani wataiba au kama wanavyosema kuwa ni kwa namna gani *watapiga cha juu.*

Mtu anakuwa na fikra kama hizi hapa hata kabla ya kuanza kazi. Ebu fikiria kama mwanachuo mwenye fikra hizo akiwa bado chuoni. Pengine mtu wa aina hiyo akikosa ajira

hapaswi kuhurumiwa kwa sababu akili yake haikuwa kama ya Diamond. Aliwaza kuiba badala ya kuwaza kuongeza thamani kwenye kile ambacho alikuwa anaenda kufanya. Ikumbukwe kuwa Akili Ya Diamond inakuhitaji wewe kufanya kitu kwa ubora wa hali ya juu sana hata kama sio cha kwako.

## 5. AKILI YA DIAMOND INAKUHITAJI WEWE KUJITUMA

Pengina unaweza kudhani kuwa Diamond analala tu, na asubuhi mambo yanajipanga. Jibu ni ndio na hapana. Jibu ni ndio kuwa mambo yanajipanga ila kwa sababu alishayapangilia huko nyuma.

Na jibu ni hapana kwa sababu yeye anapaswa kuwatafuta watu, anapaswa kufikiri mawazo mapya ya nyimbo

ambazo zitakonga nyoyo za watu.

Anapaswa kujituma kwenda kwenye *show* mbalimbali. kuna kipindi unaweza kukuta karibia wiki nzima au zaidi ya pale ana kazi. yuko kwenye mizunguko na kwenye majukwaa. Sasa hapo ndio unataka kusema vitu vinakuja kirahisi kweli?

Hapa kuna kujituma kwa hali ya juu nyuma yake. Kuna wakati wewe unakuwa umelala fofofo hujielewi, ila yeye bado

yuko kazini. Na hii ndio Akili Ya Diamond

Unaweza kupata kitabu chote mpaka mwisho kwa KUBONYEZA HAPA

Mwandishi pia anaandaa masomo kila siku kupitia YOUTUBE, SUBSCRIBE leo KWENYE CHANNEL yake kwa KUBONYZA HAPA

# HITIMISH0-1

Baada ya kuwa umesoma kitabu hiki hapa ningependa nikuulize swali moja wewe. Je, ungependa kuwa na Akili Ya Diamond?

Naomba uandike jibu lako chini kisha ulinganishe jibu hili unalotoa hapa na lile ambalo uliandika mwanzoni mwa kitabu hiki hapa.

# HITIMISHO-2

Kama kwa vyovyote vile utaamua kushirikisha kitu chochote kile ulichojifunza kwenye hiki kitabu. Basi ukikiweka kwenye mitandao ya kijamii, mwisho weka hashtag ya #akiliyaDiamond kisha nitag mimi

Instagram:@godius-_rweyongeza kwa mtandao wa

YOUTUBE: jina ni Godius Rweyongeza au bonyeza HAPA ili kusubscribe

#akiliyaDiamond

Umepata kipande hiki cha bure kabisa. unaruhusiwa pia kukisambaza kwa watu wengine pia. Ukitaka kupata kitabu kizima, basi BONYEZA HAPA Ili upate nakala yote ya kitabu.